BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MSWADA WA SHERIA YA KUREKEBISHA SHERIA MBALI MBALI NA KUWEKA MASHARTI BORA NDANI YAKE

Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuanza kuwasilisha Hotuba hii kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, Muumba wa Mbingu na Ardhi na vyote vilivyomo kwa kutujaalia uhai na afya njema ambayo imetuwezesha kutekeleza majukumu yetu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu Azidi kutujaalia amani na upendo, busara na hekima, pamoja na neema zake zote ambazo ni muhimu sana katika maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, Napenda pia, kukushukuru wewe binafsi, kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika Mkutano huu wa Tano wa Baraza hili tukufu katika kuuchangia na kuuboresha Mswada wa Sheria ya Kurekebisha Sheria Mbali Mbali na Kuweka Masharti Bora Ndani Yake. Tunamuomba Mwenyezi Mungu Mtukufu akuzidishie hekima na busara katika kutekeleza majukumu yako ya kila siku.

Mheshimiwa Spika, aidha, pongezi za dhati kabisa ziende kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali Mheshimiwa Dkt. Mwinyi Talib Haji pamoja na

watendaji wote wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar kwa ushirikiano wao mkubwa kwa Kamati wakati Kamati ilipokuwa ikijadili Mswada huu kwa muda wa siku mbili na kufikia makubaliano ya pamoja.

Mheshimiwa Spika, pia, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa mashirikiano yao makubwa waliyotoa kwangu na juhudi zao wakati wa kuujadili kwa kina Mswada huu.

Naomba sasa kwa ruhusa yako niwatambulishe Wajumbe wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa majina kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Hassan Khamis Hafidh	Mwenyekiti
2.	Mhe. Mtumwa Peya Yussuf	Makamu Mwenyekiti
3.	Mhe. Machano Othman Said	Mjumbe
4.	Mhe. Suleiman Makame Ali	Mjumbe
5.	Mhe. Salma Mussa Bilal	Mjumbe
6.	Mhe. Mohammed Mgaza Jecha	Mjumbe
7.	Mhe. Zaina Abdalla Salum	Mjumbe
8.	Ndg. Ali Alawy Ali	Katibu
9.	Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir	Katibu
10.	Ndg. Amina Abeid Hemed	Mkalimani wa Lugha za

Alama

Mheshimiwa Spika, sina budi kueleza kuwa, Mswada huu ni marekebisho ya baadhi ya vifungu katika sheria mbali mbali, ambapo vingi kati ya vifungu hivyo vinafanyiwa marekebisho ya kuvirudisha katika sheria zao za awali baada ya Serikali kuona ipo haja ya kufanya hivyo. Pia, maelezo zaidi ya mapendekezo hayo yanaonekana katika Marekebisho ya Kamati ambayo Waheshimiwa Wajumbe tayari mmeshapatiwa kwa ajili ya ufafanuzi na ufahamu zaidi.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kufuta katika Mswada huu *kifungu cha 11* chenye marekebisho ya kuongezwa *kifungu kipya cha 23*C katika sheria mama. Kamati imefikia makubaliano hayo baada ya kuona mantiki ya kifungu hiki na changamoto za kisheria ambazo zitajitokeza siku za baadae.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuangalia utaratibu bora ambao utawezesha malengo ya kifungu hiki kuweza kufikiwa kwa kufanya utafiti wa kina juu ya changamoto ambazo zimepelekea kuanzishwa kwa Polisi wa Utalii na Diplomasia katika sekta ya Utalii, kwa vile uanzishwaji wa Polisi wa Utalii na Diplomasia limeingia katika masuala ya Muungano na mamlaka hayo yapo kwa Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na si mamlaka ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyofahamu kwamba Zanzibar imejitangaza kitaifa na kimataifa kuimarisha soko lake la utalii na muitiko mkubwa wa mataifa umepatikana na wenye tija kwa nchi yetu. Kwa mnasaba huo, Kamati inapendekeza kwamba katika kuuendeleza Mji Mkongwe ambao ni

kivutio muhimu cha utalii kuwekwa utaratibu nzuri wa kuendesha shughuli zote za kiuchumi na kijamii kwa misingi ya sheria za nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Aidha, Kamati inashauri kufanywa marekebisho ya kifungu cha 18 cha Mswada huu ambacho kimebeba marekebisho ya kifungu cha 7 cha sheria mama baada ya kifungu hiki kutoa mwanya wa kuharibu Utamaduni, Mila na Silka za Kizanzibari. Hivyo, katika aya mpya iliyoongezwa Kamati inashauri kusomeka kama ifuatavyo:

"(g) kuruhusu uwekezaji wowote wa kibiashara, makaazi na shughuli nyengine yoyote ndani ya Mji Mkongwe wa Zanzibar kwa kuzingatia sheria za nchi na Mpango Mkuu wa Uhifadhi na Urithi wa Mji Mkongwe;"

Mheshimiwa Spika, aidha, Kamati inashauri Mfuko ulioanzishwa katika Sheria hii ambao umeweka asilimia tano (5%) ya mapato ya miundombinu kuingia katika mapato ya Uhifadhi wa Mji Mkongwe yaende yakatumike kwa uadilifu na kwa malengo yaliyokusudiwa. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga fedha hizo kwa ajili ya mapato ya Mfuko wa Mji Mkongwe kwani kwani kuanzishwa kwa Mfuko huo kutasaidia kuimarisha huduma za kijamii kama vile vyoo katika maeneo haya. Vile vile, fedha nyingi zinahitajika kwa ajili ya kuendeleza miundombinu pamoja na kukuza sekta ya Utalii kupitia kivutio hiki adhim katika nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri kufanywa marekebisho mapya ya *kifungu cha 2* cha Sheria Mama ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, *Nam. 5 ya*

2019 kwa kufutwa na kuandikwa upya tafsiri ya maneno *"Wiki ya kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa"* kama ifuatavyo:

"Wiki ya kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, Waasisi wa Mapinduzi ya Zanzibar na Katibu wa Kwanza wa Chama cha Afro Shirazi" Maana yake ni wiki inayoanzia tarehe 1 hadi 6 Aprili ya kila mwaka.

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe hotuba yangu kwa kuwashauri wajumbe wa Baraza lako Tukufu wakubaliane na maoni ya Kamati yetu katika Mswada huu kwani Kamati imepata mafunzo ya kutosha kupitia wataalamu wetu wa Baraza lengo la kuiwezesha Serikali kuzifanyia marekebisho Sheria hizi ili iwe nyenzo muhimu katika kufanikisha majukumu yao.

Mheshimiwa Spika, vile vile, Kamati yetu inawaomba Wajumbe wa Baraza hili Tukufu waujadili na kuuchangia ipasavyo Mswada huu na hatimae kuupitisha ili kuwa sheria ambayo itaziwezesha Taasisi hizi kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Naomba Kuwasilisha.

Ahsante,

.....

(*Mhe. Hassan Khamis Hafidh*)

Mwenyekiti,

Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,

BARAZA LA WAWAKILISHI,

ZANZIBAR